*Mulika, Na. 41 (1), 110-125*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# Raha na Karaha ya Uradidi wa Vitabu vya Fasihi kwa Shule za Sekondari Nchini Tanzania

*Newaje Ali Mganga*[1]
Chuo Kikuu cha Sumait-Zanzibar

DOI: https://doi.org/10.56279/mulika.na41t1.8

**Ikisiri**

Mihtasari ya vidato vya tatu hadi sita kupitia ujuzi wa jumla na malengo ya ufundishaji wa somo la Kiswahili kwa shule za sekondari nchini Tanzania, imetoa mwongozo murua kuhusu utekelezaji wake. Kwa upande wa sarufi, mambo yamenyooka si haba, kwani mwalimu ana fursa ya kutoa mifano kulingana na mazingira ya darasa lake. Changamoto inayojitokeza ni katika upande wa mada za fasihi, kwani kuna mazoea ya kujirudiarudia kwa matumizi ya vitabu vya kibunilizi: diwani, riwaya na tamthiliya, licha ya kuwapo kwa vitabu vya kutosha katika uwanja huo. Suala hilo husababisha raha na karaha katika mustakabali wa wahitimu watarajiwa. Hivyo, makala haya yamenuia kudadisi raha na karaha hizo katika ustawi wa fasihi ya Kiswahili katika jamii. Ikumbukwe kwamba wanafunzi wa leo ndio wanafasihi wa kesho katika kuzitunga, kuzihakiki na kuzichambua kazi mbalimbali za fasihi ya Kiswahili. Kuandaliwa mazingira mazuri katika kujifunzi kutawezesha kupata wahitimu wenye uwezo wa kuhimili na kuhudumu nafasi hizo kwa weledi na uaminifu.

## 1.0 Utangulizi

Historia ya ufundishaji wa fasihi ya Kiswahili nchini Tanzania imeanza katika miaka ya 1960 kwa ngazi ya kidato cha nne tu, chini ya usimamizi wa mitihani ya Cambridge. Huku upande wa vidato vya tano na sita ilianza kufundishwa muongo mmoja baadaye tena kwa baadhi ya shule za sekondari, kama asemavyo Mulokozi (2019) kwamba kuasisiwa kwa masomo ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 1967-1970, kuliibua hitajio la kuanzishwa pia masomo hayo katika shule za sekondari, ili kupata wanafunzi watakaojiunga na chuo kikuu wakiwa na msingi wa Kiswahili tokea chini. Kwa hivyo, mwaka 1970 rasmi masomo ya Kiswahili yakaanza kufundishwa katika kidato cha tano na sita kwa baadhi ya shule za sekondari, yaani shule ya Mkwawa kwa ajili ya wavulana na Korogwe kwa ajili ya wasichana.

Kwa mujibu wa Mulokozi (*keshatajwa*) uanzishaji huo wa masomo ya Kiswahili katika shule hizo, ulikabiliwa na changamoto kuu nne: wahitimu kuhofia kupata ajira, uhaba wa walimu wenye sifa za kufundisha ngazi hiyo, uhaba wa vitabu vya

[1] **Baruapepe:** nawajea@gmail.com

marejeleo hasa vya fasihi na uhaba wa istilahi, uliotokana na taaluma hii kuwa ndio kwanza ilikuwa inamea. Hatimaye, changamoto zote zilitafutiwa ufumbuzi na somo la Kiswahili likafundishwa ingawa kwa kusuasua.

Ifahamike kuwa katika ufundishaji huo wa somo la Kiswahili, ndani yake kulikuwa na ufundishaji wa sarufi na fasihi kwa ngazi ya shule za sekondari. Hivyo, licha ya kusuasua kwa mchakato wa ufundishaji, mafanikio yalipatikana kidogokidogo kutokana na nia na dhamira ya dhati iliyokuwapo. Kutokana na ushirikiano uliokuwapo baina ya shule za sekondari zilizokuwa zikifundisha somo la Kiswahili na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, fasihi ya Kiswahili ilikua na kuenea maeneo mbalimbali duniani. Katika hili Mulokozi anasema:

> Mchakato wa kuasisiwa kwa taaluma ya Fasihi nchini Tanzania ambao tumeuelezea ulikuwa na taathira au matokeo makubwa katika maendeleo ya fasihi ya Kiswahili na taaluma yake. Athari kubwa kuliko zote ilikuwa ni kuwezesha kupanuka na kuenea kwa taaluma ya fasihi ya Kiswahili ndani na nje ya Tanzania. Taaluma hiyo iliendelezwa kwa njia ya mijadala, machapisho na wataalamu (Mulokozi, 2019:26).

Nukuu hiyo inaonesha mafanikio yaliyofikiwa baada ya juhudi za miongo mitano ya kuasisiwa kwa ufundishaji wa somo la fasihi ya Kiswahili nchini Tanzania. Chanzo chake kikiwa ni maandalizi imara ya shule za sekondari na mwendelezo wake chuo kikuu. Hivyo, katika kulidumisha hilo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa nia njema, ilianzisha Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ikiwa na jukumu la kufasiri sera ya elimu nchini na kuziweka katika mitaala ya kujifunzia ili kutoa elimu bora katika ngazi za elimu ya awali, msingi, sekondari na vyuo vya ualimu. TET ilianzishwa kwa Sheria Na. 13 ya mwaka 1963 na kuitwa Taasisi ya Elimu, baadaye ilibadilishwa jina na kuitwa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) kwa Sheria ya Bunge Na. 5 ya mwaka 1993.

Mtaala wa elimu hulenga mambo kadhaa kwa wahitimu wake. Kwa mantiki hiyo, ni matarajio yetu kuwa mihtasari ya somo la Kiswahili ya kidato cha tatu hadi cha sita kwa shule za sekondari nchini Tanzania imelitilia mkazo suala la kuzalisha wahitimu bora. Katika kulishughulikia hilo, mihtasari ya kidato cha tatu na nne (2010) na kidato cha tano na sita (2010) imeorodhesha malengo ya kufundisha somo la Kiswahili kwa shule za sekondari nchini Tanzania, miongoni mwa malengo hayo ni:

i. Kujenga tabia ya udadisi na ubunifu katika masuala ya lugha na fasihi ya Kiswahili;
ii. Kuelewa, kuthamini na kutumia kazi za fasihi katika maisha;
iii. Kutumia lugha ya kisanii katika miktadha mbalimbali;
iv. Kujenga tabia ya kusoma maandiko mbalimbali ya Kiswahili;

v. Kupata msingi bora na imara wa kujifunza na kujiendeleza; na
vi. Kutumia Kiswahili kupata maarifa, mwelekeo, na stadi za kijamii, kitamaduni, kiteknolojia na kitaaluma kutoka ndani na nje ya nchi.

Hayo ni baadhi tu ya malengo ya kufundisha somo la Kiswahili kwa shule za sekondari nchini Tanzania, kuanzia kidato cha tatu hadi cha sita. Tumechagua yanayoendana na fasihi ili kuonesha athari ya uradidi wa vitabu vya bunilizi katika kufikia ujuzi wa jumla na malengo hayo. Hii ni kwa sababu ufanisi wa mtaala ni kufanikiwa kwa malengo ya mtaala kwa wahitimu wa elimu lengwa. Kwa muktadha wa makala haya, tumerejelea kufanikiwa kwa malengo ya mtaala kwa wahitimu wa somo la Kiswahili, na hasa upande wa fasihi, katika ngazi ya kidato cha nne na kidato cha sita. Hivyo, ili kuweza kueleza iwapo mitaala imefanikiwa au la, ni muhimu kulinganisha malengo yaliyoorodheshwa na mihtasari ya vidato husika na matokeo ya wahitimu. Kinacholinganishwa hapa siyo tu matokeo ya mitihani bali pia matokeo ya kimaisha. Hii ina maana kuwa tutaangalia ni kwa kiasi gani wahitimu hao wamemudu kukabiliana na maisha katika kuzitumia fursa zinazotokana na fasihi. Mathalani, wangapi wamekuwa watunzi, wahakiki, wahariri na wachambuzi wa kazi za fasihi katika maisha halisi? Swali kama hili lilishawahi kufanyiwa utafiti na majibu yake yakawa kama ifuatavyo:

> Walimu na wanafunzi waliombwa kuonesha ni kwa kiwango gani mtaala wa elimu wa Tanzania unafaa katika kutoa wahitimu mahiri, wenye kujiamini, wanaowajibika na wenye ujuzi unaohitajika. Matokeo yanaonesha, idadi kubwa ya washiriki, walimu na wanafunzi, walisema kwamba mtaala wa elimu wa Tanzania hauna uwezo wa kutoa wahitimu mahiri katika nyanja mbalimbali. Kwa mfano, ni asilimia 35 tu ya walimu na asilimia 26 ya wanafunzi ndiyo walioripoti kwamba mtaala unafaa katika kuandaa wahitimu mahiri na wenye kujiamini. (Zombwe, 2011:2).

Matokeo ya utafiti wa Zombwe (*keshatajwa*) yanaonesha dosari za mitaala ya elimu nchini Tanzania. Hivyo, kuna haja kubwa ya kulidadisi suala la raha na karaha ya uradidi wa vitabu vya fasihi kwa shule za sekondari nchini Tanzania ili kubainisha jinsi linavyoathiri ufanisi katika utekelezaji wa mitaala.

## 2.0 Dhana ya Uradidi wa Vitabu vya Fasihi

Istilahi uradidi wa vitabu vya fasihi kama inavyotumika katika utafiti huu, inamaanisha hali ambayo vitabu vya fasihi vinatumika kwa muda mrefu bila kubadilishwa. Hali hii inaitwa uradidi kwa kuwa vitabu hivyo vitajirudiarudia na kutumika kujibia mitihani husika kwa kipindi kirefu bila kubadilishwa.

Nchini Tanzania, uradidi wa vitabu ni suala ambalo limekuwapo kwa muda mrefu. Kwa mfano, kwa mujibu wa Mulokozi (2019) orodha ya vitabu teule katika miaka ya 1960, iliishia kidato cha nne, ambapo kulikuwa na riwaya za F. Katalambula, M.

S. Abdulla, S. Robert, J. Mbotela. Aidha, kulikuwa na tamthiliya za H. Kuria, G. Hyslop, G. Ngugi, na baadaye E. Hussein na J. Nyerere. Kwa upande wa ushairi, kulikuwa na diwani za S. Robert, A. Abedi, M. Mnyampala, K.H.A. Akilimali, Z. Zani, H. Cory na washairi wengine. Kwa miaka ya hivi karibuni vitabu vilivyotumika ni kama ilivyobainishwa katika majedwali Na. 1-3 chini:

**Jedwali Na. 1: Orodha ya Vitabu vya Fasihi Vilivyotumika katika Shule za Sekondari Miaka ya 2000-2004**

| Na. | Utanzu | Kitabu | Mwandishi |
|---|---|---|---|
| **Kidato cha 3-4** | | | |
| 1. | Ushairi | A. *Diwani ya Mloka*<br>B. *Diwani ya Ustadhi*<br>C. *Malenga Wapya* | C. Mloka<br>A. Andanenga<br>TAKILUKI |
| 2. | Tamthiliya | A. *Hawala ya Fedha*<br>B. *Mfalme Juha*<br>C. *Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe* | A. Lihamba,<br>F. Topan<br>E. Semzaba |
| 3. | Riwaya | A. *Hiba ya Wivu*<br>B. *Kusadikika*<br>C. *Zawadi ya Ushindi* | Z. Mwanga<br>S. Robert,<br>B. Mtobwa |
| **Kidato cha 5-6** | | | |
| 4. | Ushairi | A. *Kimbunga*<br>B. *Mapenzi Bora*<br>C. *Chungu Tamu*<br>D. *Wasakatonge* | H. Gora<br>S. Robert<br>T. Mvungi<br>M. Khatib |
| 5. | Tamthiliya | A. *Kwenye Ukingo wa Thim*<br>B. *Morani*<br>C. *Kivuli Kinaishi*<br>D. *Nguzo Mama* | E. Hussein<br>E. Mbogo<br>S. Mohamed<br>P. Mhando |
| 6. | Riwaya | A. *Pesa Zako Zinanuka*<br>B. *Barua Ndefu Kama Hii*<br>C. *Janga Sugu la Wazawa*<br>D. *Vuta N'kuvute* | B. Mtobwa<br>Mariam Ba<br>G. Ruhumbika<br>A. Shafi |

**Chanzo:** Mitihani ya Taifa (2000-2004)

Vilevile, uradidi wa vitabu vya fasihi nchini Tanzania umeonekana katika miaka ya 2005 hadi 2008. Katika miaka hiyo, vitabu vya fasihi vilivyokuwa vinatumika katika mitihani ya kidato cha nne na sita ni vilevile. Vitabu hivyo vimewasilishwa katika Jedwali Na. 2 lifuatalo:

**Jedwali Na. 2: Orodha ya Vitabu vya Fasihi Vilivyotumika katika Shule za Sekondari Miaka ya 2005-2008**

| Na. | Utanzu | Kitabu | Mwandishi |
|---|---|---|---|
| **Kidato cha 3-4** | | | |
| 1. | Ushairi | A. *Diwani ya Mloka*<br>B. *Mashairi ya Cheka Cheka*<br>C. *Malenga Wapya* | C. Mloka<br>T. Mvungi<br>TAKILUKI |
| 2. | Tamthiliya | A. *Kilio Chetu*<br>B. *Mfalme Juha*<br>C. *Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe* | A. Medical Aid Foundation<br>F. Topan<br>E. Semzaba |
| 3. | Riwaya | A. *Kiu ya Haki*<br>B. *Kusadikika*<br>C. *Watoto wa Maman'tilie* | Z. Mwanga<br>S. Robert<br>E. Mbogo |
| **Kidato cha 5-6** | | | |
| 4. | Ushairi | A. *Kimbunga*<br>B. *Mapenzi Bora*<br>C. *Chungu Tamu*<br>D. *Wasakatonge* | H. Gora<br>S. Robert<br>T. Mvungi<br>M. Khatib |
| 5. | Tamthiliya | A. *Kwenye Ukingo wa Thim*<br>B. *Morani*<br>C. *Kivuli Kinaishi*<br>D. *Nguzo Mama* | E. Hussein<br>E. Mbogo<br>S. Mohamed<br>P. Mhando |
| 6. | Riwaya | A. *Pesa Zako Zinanuka*<br>B. *Barua Ndefu Kama Hii*<br>C. *Janga Sugu la Wazawa*<br>D. *Vuta N'kuvute* | B. Mtobwa<br>Mariam Ba<br>G. Ruhumbika<br>A. Shafi |

**Chanzo:** Mitihani ya Taifa (2005-2008)

Aidha, uradidi mkubwa wa vitabu vya fasihi vinavyotumika kufundishia katika shule za sekondari nchini Tanzania umeonekana katika miaka ya 2009 hadi 2022. Katika miaka hiyo, vitabu vya fasihi ambavyo vimekuwa vikitumika katika mitihani ya kidato cha nne na sita ni vilevile. Vitabu hivyo vimebainishwa katika Jedwali Na. 3.

**Jedwali Na. 3: Uradidi wa Vitabu vya Fasihi Vinavyotumika katika Shule za Sekondari Miaka ya 2009-2022**

| Na. | Utanzu | Kitabu | Mwandishi |
|---|---|---|---|
| **Kidato cha 3-4** | | | |
| 1. | Ushairi | A. *Wasakatonge*<br>B. *Malenga Wapya* | M. Khatibu<br>TAKILUKI |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | C. *Mashairi ya Chekacheka* | T.A. Mvungi |
| 2. | Tamthiliya | A. *Orodha*<br>B. *Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe*<br>C. *Kilio Chetu* | S. Raynolds<br>E. Semzaba<br>Medical Aid Foundation |
| 3. | Riwaya | A. *Takadini*<br>B. *Watoto wa Mama N'tilie*<br>C. *Joka la Mdimu* | B.J. Hanson<br>E. Mbogo<br>A.J. Safari |
| **Kidato cha 5-6** | | | |
| 4. | Ushairi | A. *Kimbunga*<br>B. *Mapenzi Bora*<br>C. *Chungu Tamu*<br>D. *Fungate ya Uhuru* | H. Gora<br>S. Roberts<br>T.A. Mvungi<br>M.S. Khatib |
| 5. | Tamthiliya | A. *Kwenye Ukingo wa Thim*<br>B. *Morani*<br>C. *Kivuli Kinaishi*<br>D. *Nguzo Mama* | E. Hussein<br>E. Mbogo<br>S. Mohamed<br>P. Muhando |
| 6. | Riwaya | A. *Usiku Utakapokwisha*<br>B. *Kufikirika*<br>C. *Mfadhili*<br>D. *Vuta n'Kuvute* | M. Msokile<br>S. Roberts<br>H. Tuwa<br>A. Shafi |

**Chanzo:** Mitihani ya Taifa (2009-2022)

Katika Jedwali Na. 3 uradidi wa vitabu vya fasihi unabainika kuwapo kwa zaidi ya muongo mmoja. Katika kipindi cha miaka hiyo, vitabu vya fasihi vimeendelea kuwa vilevile bila kubadilishwa. Kwa mantiki hiyo, ijapokuwa uradidi wa vitabu vya fasihi umebainika kuwapo kwa miaka mingi, katika makala haya tutajikita katika uradidi wa kuanzia mwaka 2009-2022. Uteuzi huo umetokana na matumizi ya vitabu hivyo kudumu kwa muda mrefu zaidi katika kipindi hiki ambacho ndicho sasa. Athari za uradidi huo zinaweza kutabiri mustakabali wa wahitimu wa somo la Kiswahili na fasihi kwa upekee katika kukabiliana na vikwazo vya maisha ya kila siku.

## 3.0 Kiunzi cha Nadharia

Utafiti wa makala haya uliongozwa na Nadharia ya Uhalisia. Nadharia ya Uhalisia ilichagizwa na Karelis (1979) kupitia kitabu chake cha *Hegel's Introduction to Aesthetics*. Katika kitabu hicho anasisitiza matumizi ya uhalisia katika kuelezea kazi za kifasihi zinazowasilisha maisha ya jamii kupitia matendo ya wahusika yanayosawiri waziwazi hali iliyomo. Karelis (*keshatajwa*) anadai kwamba nadharia hii iliasisiwa katika karne ya kumi na tisa na kufafanuliwa zaidi na Groffman mwaka 1952. Kwa mujibu wa Ntarangwi (2004), nadharia hii hujikita katika uwakilishi wa uhalisi wa mambo katika fasihi kupitia jamii lengwa. Nadharia hii iliibuliwa katika juhudi za kupinga mkondo wa kiulimbwende.

Uhalisia unajikita katika matokeo ya mambo na ukweli unaoweza kuonekana na/au kuthibitishwa na tajiriba. Nadharia hii huchunguza jinsi mwandishi alivyo-uwasilisha uhalisia wa mambo kupitia maudhui yake. Mwanafasihi hana budi kusawiri wahusika, matukio na mandhari yanayokubalika na kuaminika katika jamii kwa minajili ya kuibua maudhui lengwa. Kwa mantiki hiyo, vipengele vya fani na maudhui katika kazi ya fasihi, lazima viendane na hali halisi na maisha ya kawaida kwani sanaa inapaswa ihalisike.

Dhana ya uhalisia hutumika kuakisi sifa za kimsingi zinazohusishwa na muktadha wa kijamii. Kama asemavyo Wafula (2007), uhalisia unahusishwa na kipindi maalumu kihistoria katika jamii za Ulaya. Kipindi hiki kinahusishwa na waandishi kama vile Balzac, Stendhal na Flaubert. Waandishi hawa wanasisitiza maelezo ya ukweli katika kazi zao na waliamini kuwa dhima ya mwandishi ni kuonesha ukweli jinsi ulivyo. Fasihi yoyote lazima ionekane kama kioo cha jamii. Hivyo basi, ni lazima jamii iweze kujitazama na kujiona kupitia fasihi.

Katika makala haya, dhima ya Nadharia ya Uhalisia ilisaidia kubainisha ukweli wa raha na karaha ya uradidi wa vitabu vya fasihi kwa shule za sekondari nchini Tanzania kwa wakati wa sasa kwani kwa mujibu wa nadharia hii, kazi ya fasihi inapaswa kuwasilisha ukweli kama ulivyo katika muktadha wake. Pia, kazi ya fasihi inapaswa iangalie changamoto na kuchunguza chanzo chake. Hivyo, raha ni ule ubora wa uradidi na karaha ni ule udhaifu wa uradidi huo kwa wahitimu wa leo katika jamii ya Kitanzania ya utandawazi.

## 4.0 Methodolojia ya Utafiti

Utafiti uliozaa makala haya umejikita katika kutumia data ya vitabu radidi vya fasihi andishi ya Kiswahili, kwani tayari vilikwishadumu kwa zaidi ya muongo mmoja. Wango la utafiti lilijumuisha vitabu teule vya fasihi katika shule za sekondari nchini Tanzania, watunzi wa kazi za fasihi, walimu wa Kiswahili wa shule za sekondari pamoja na wahitimu wa kidato cha nne na cha sita. Sampuli ilihusu waandishi wa kazi za fasihi wawili, mmoja kazi yake ikiwamo katika orodha ya vitabu teule na mmoja kazi zake si miongoni mwa vitabu teule. Waandishi hawa walichaguliwa ili kupata maoni kuhusu suala hili la uradidi wa vitabu. Aidha, kutumiwa kwa mwandishi ambaye kazi yake ni miongoni mwa kazi teule na yule ambaye kazi zake si miongoni mwa kazi hizo, kuliwezesha kupata maoni tofauti ya waandishi kuhusu suala hili. Pia, ilihusisha walimu wawili, mmoja wa kidato cha nne na mwingine wa kidato cha sita, kwa kuwa wao ndio wafundishaji wa vitabu teule pamoja na wahitimu sita wa shule za sekondari, watatu kwa kila kidato, kwa kuwa wao ndio walengwa wakuu wa vitabu hivyo. Waandishi, walimu na wanafunzi hao, waliteuliwa kwa sababu ndiyo wadau wakuu wa uradidi wa vitabu hivyo. Vitabu vya fasihi vya shule za sekondari nchini Tanzania, kidato cha tatu

hadi cha sita 2009-2022 ndio vilivyochaguliwa na mtafiti. Mtafiti aliteua sampuli hii kutokana na malalamiko ya baadhi ya waandishi wa vitabu vya fasihi kuhusu hali ya uradidi iliyodumu kwa muongo mzima.

Data zilizopatikana kutoka kwa watoatarifa hao zilisaidia kubainisha raha na karaha za uradidi wa vitabu vya fasihi kwa shule za sekondari Tanzania. Data hizo zilinasibishwa na mustakabali wa wahitimu, usanisi wa ufundishaji wa walimu na tija ya waandishi wa vitabu na fasihi ya Kiswahili kwa ujumla. Njia kuu ya kukusanya data ilikuwa ya mjadala wa vikundi lengwa vinne kwa mujibu wa tahasusi zao, yaani kulikuwa na vikundi viwili vya wahitimu (wahitimu 6, watatu kwa kila kidato), kikundi kimoja chenye walimu wawili pamoja na kikundi kimoja kilichojumuisha waandishi wawili. Katika mchakato huo wa ukusanyaji wa data, mwongozo wa mjadala wa vikundi lengwa ulilenga kubainisha raha na karaha wanayoipata kupitia uradidi huo.

## 5.0 Uwasilishaji wa Matokeo

Matokeo ya utafiti yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo yaliyohusu jinsi raha na karaha za uradidi wa vitabu teule vya fasihi kwa shule za sekondari nchini Tanzania zinavyoibuka. Kwa njia ya maelezo, mtafiti aliorodhesha raha za uradidi wa vitabu teule vya fasihi kwa shule za sekondari nchini Tanzania. Pia, mtafiti alibainisha karaha za uradidi wa vitabu teule vya fasihi kwa shule za sekondari nchini Tanzania. Mifano ilinukuliwa ili kudokeza majibu ya watoataarifa kuhusu raha na karaha za uradidi wa vitabu teule vya fasihi kwa shule za sekondari nchini Tanzania kwa mujibu wa malengo ya utafiti na dhima ya nadharia teule.

### 5.1 Raha ya Uradidi wa Vitabu

Matokeo ya utafiti wa makala haya yalibaini kwamba uradidi wa vitabu vya fasihi ya Kiswahili nchini Tanzania, kwa zaidi ya muongo mmoja, una raha zinazojumuisha usahali wa kupata vitabu teule, chanzo cha mapato kwa mwandishi, kumpa tajiriba mwalimu, kuziba mwanya wa rushwa, na kuongeza kiwango cha ufaulu wa somo la Kiswahili. Ufuatao ni ufafanuzi wa raha hizo kutokana na mwongozo wa dhima ya Nadharia ya Uhalisia isemayo, kazi ya fasihi iwasilishe ukweli kama ulivyo katika muktadha wake na iangalie changamoto na kuchunguza chanzo chake.

#### 5.1.1 Usahali wa Kupata Vitabu Teule

Kwa kuwa tangu mwaka 2009-2022, vitabu teule ni vilevile, ni wazi kuwa kila nyumba yenye mwanafunzi aliyewahi kusoma kidato cha 3-4 au cha 5-6 inatarajiwa kuwa na vitabu teule. Vitabu hivyo vinatazamiwa kutoadimika katika mazingira ya jamii ya Kitanzania kwani vimetumika kwa muda mrefu. Hii ina maana kwamba, kwa kuwa vitabu hivyo vimetumika kwa miaka mingi na kuna umuhimu wa kila mwanafunzi kuwa navyo, kila anayesoma vidato hivyo hana budi kuvipitia vitabu

teule. Vitabu hivyo alisomea baba, mtoto na mjukuu pia watavitumia. Katika kulishadidia hilo mtoataarifa anasema:

> Kiukweli vitabu teule vya kidato cha tatu mpaka cha sita, vimejaa tele shuleni na hata majumbani. Hii ni kwa sababu kila mwaka vinatahiniwa hivyohivyo, kiasi cha kusema alichosomea kaka, ndugu na dada ni hichohicho.
> **Chanzo:** Data za Uwandani, 2019.

Maelezo haya yanathibitisha kuwa kutokana na kutumika kwa miaka mingi, upatikanaji wa vitabu teule umekuwa rahisi. Hii ni kwa sababu mwanafunzi anaweza kutumia kitabu alichotumia dada au kaka yake (yaani mtumba). Kwa sababu hiyo, hata familia zenye uwezo duni ambazo hazimudu kununua vitabu vipya kila mwaka, zinaweza kuepuka gharama kwa kuendelea kutumia vitabu vilivyotumiwa na mwanafunzi aliyehitimu. Kwa minajili hiyo, utunzaji wa vitabu hivyo unahitajika ili kuvifanya viweze kutumika kwa siku za usoni. Vilevile, hata shule zenye maktaba dhaifu pia zinaweza kudiriki kuwa navyo vitabu hivyo kutokana na kurejewa kila mwaka.

Mbali na hilo, kutokana na uhakika wa soko, uzalishaji wa vitabu vyenye uradidi huwa mkubwa sana. Hivyo, upatikanaji wake huwa rahisi na kurahisisha upatikanaji wa marejeleo kwa wanafunzi.

### 5.1.2 Chanzo cha Mapato kwa Mwandishi

Kimapato, uandishi una mchango wake katika uchumi wa mwandishi husika na nchi kwa ujumla. Ubidhaishaji vitabu unatengeneza ajira kwa mtu binafsi, taasisi na mashirika mengine. Kwa muktadha huo, uandishi wa kazi za kifasihi ambazo huweza kutumiwa katika mitaala ya shule za sekondari, hukuza pato la mwandishi litokanalo na uuzaji wa vitabu teule. Kadiri wanafunzi wanavyokuwa wengi, ndivyo mapato yanavyoongezeka. Mapato yanaongezeka kwa sababu takribani wanafunzi wa Tanzania nzima, wa vidato vya mitihani, hutumia vitabu hivyo. Kwa kuwa, vitabu vyenyewe hudumu kwa zaidi ya muongo mmoja, kimahesabu, waandishi wa vitabu teule wanatarajiwa kupata donge nono katika mauzo ya vitabu vyao. Mtoataarifa mmoja alikuwa na haya ya kusema:

> Jambo la mapato siyo sana lakini hamna hamna ndimo mliwamo. Binafsi napata chochote, lakini si kusema kuwa napata. Nashukuru huko kukumbukwa kwa iyo asilimia ngapi sijui, ila ndiyo napata si kukaa bure... unajua kazi ya uandishi kwa huku kwetu bado hajawa ya kulipa sana.
> **Chanzo:** Data za Uwandani, 2019.

Maelezo hayo, ingawa hayaoneshi kuridhika na kipato cha mauzo ya vitabu, bado yanadokeza kuwa ‘haba na haba hujaza kibaba’, kama wahenga walivyosema. Labda kwa waandishi waliochapisha kwa pesa zao wenyewe wanaweza kuwa

wanapata faida ya kutosha. Jambo la muhimu ni kwamba kupata si kukosa kabisa, kwani hata kama wanapata kidogo lakini mkono wa mwandishi unapata kwenda kinywani.

### 5.1.3 Mwalimu Kupata Tajiriba

Uradidi wa bunilizi katika shule za sekondari, huwafanya walimu kuzoea fani na maudhui yake na kuwafanya wawe na tajiriba ya kutosha katika ufundishaji wa kazi hizo za kifasihi. Hii ni kwa sababu, kwa zaidi ya muongo mmoja wanafundisha kitu hichohicho. Hata hivyo, kufundisha ni taaluma, hivyo, inahitaji maandalizi wakati wote. Mwalimu akiwa amefanya maandalizi ya kutosha kabla ya kuingia darasani kufundisha huleta ufanisi halisi. Mtoataarifa alisema:

> Mimi huu ni mwaka wangu wa kumi katika tasnia ya ualimu. Nimekuwa nikifundisha fasihi mara zote hizo. Pia, nimekuwa mzoefu na vitabu kwani nimeshavikariri kiasi cha kutohitaji maandalizi makubwa kabla ya kuingia darasani. Nafikiri tangu nimeanza kufundisha vitabu havijabadilishwa
> **Chanzo:** Data za Uwandani, 2019.

Hii ni kusema kuwa walimu walioanza kufundisha muongo mmoja uliopita, sasa wamekuwa wakongwe na wamevizoea vitabu teule katika mtaala wa sasa. Jambo hilo linawaletea wepesi katika mchakato wa kufundisha. Hivyo, huwafanya kutumia muda mfupi tu kufanya maandalizi ya kufundisha. Pia, kwa upande mwingine, huwafanya wawawezeshe wanafunzi kufaulu kwa wepesi zaidi maana vitabu hivyo vimekuwa sehemu yao ya maisha. Hivyo, uradidi wa vitabu vya fasihi kwa shule za sekondari nchini Tanzania unaongeza uzoefu wa mwalimu katika ufundishaji wake.

### 5.1.4 Kuziba Mwanya wa Rushwa

Kama wahenga wasemavyo rushwa ni adui wa haki, yaani mwenye haki anaweza kudhulumiwa au kunyimwa haki yake, kiasi ambacho mambo yanaweza kwenda ndivyo sivyo. Uradidi wa vitabu vya fasihi unaziba mwanya wa rushwa kutokana na waandishi wa vitabu kutokuwa na fursa yakutoa rushwa ili vitabu vyao viingizwe kwenye orodha ya vitabu teule. Katika kulitolea ufafanuzi jambo hili, mmoja wa watoataarifa anaeleza:

> Kwa vile vitabu vya fasihi hudumu kwa muda mrefu, waandishi wengine huwa hawajitaabishi kutoa hongo, kwani aliyekuwemo kwenye orodha ana uhakika wa kudumu kwa zaidi ya miaka kumi. Hivyo, wale wenye tamaa ya kupita njia ya mkato huwa hawana namna ila wawe wapole katika mazingira hayo.
> **Chanzo:** Data za Uwandani, 2022.

Maelezo ya mtoataarifa huyo yanaonesha kuwa hali ya vitabu vya fasihi kudumu kwa zaidi ya muongo mmoja, husaidia huziba mianya ya rushwa, kwani hata mwandishi akitaka kutoa rushwa itakuwa vigumu kwa vile vitabu teule hutumika

kwa muda mrefu. Kwa mantiki hiyo, uradidi wa vitabu vya fasihi kwa shule za sekondari nchini Tanzania, unawafanya waandishi ambao vitabu vyao havimo katika orodha ya vitabu teule kuwa wavumilivu na kutojihusisha kabisa na utoaji wa rushwa, ili vitabu vyao viingizwe katika orodha teule kwani rushwa haitafanikisha hilo

### 5.1.5 Kuongeza Kiwango cha Ufaulu wa Somo la Kiswahili

Kwa miongo kadhaa, matokeo ya somo la Kiswahili kuanzia kidato cha nne hadi cha sita, yamekuwa yakiongoza kwa kuwa mazuri kuliko masomo mengine. Kwa mfano, kwa mujibu wa NECTA (2019, 2020, 2021 na 2022), watahiniwa wa somo la Kiswahili katika vidato vya nne na sita wamekuwa wakifaulu somo hilo kwa zaidi ya asilimia 90, jambo ambalo halijitokezi katika masomo mengine. Jedwali Na. 4 lifuatalo linabainisha:

**Jedwali Na. 4: Hali ya Matokeo ya Mitihani ya Kiswahili kwa Vidato vya Nne na Sita**

| Na. | Mwaka | Ufaulu wa Kidato cha Nne | Ufaulu wa Kidato cha Sita |
|---|---|---|---|
| 1. | 2019 | 91% | 100% |
| 2. | 2020 | 94% | 100% |
| 3. | 2021 | 95% | 100% |
| 4. | 2022 | - | 100% |

**Chanzo:** Taarifa za Uchambuzi wa Majibu ya Watahiniwa Kidato cha IV na VI

Hali hiyo inaweza kuwa inasababishwa na mambo mbalimbali, mmoja wa watoataarifa alidokeza:

> Unajua, wanafunzi wamekuwa wakifaulu somo la Kiswahili kuliko masomo mengine kwa sababu ndiyo uwanja wa nyumbani... kwa kuwa vitabu wanavyojibia ndio hivyo kwa hivyo; kuna tahakiki za kutosha. Lakini hata walimu wao wanamudu kuvifundisha vitabu hivyo.
> **Chanzo:** Data za Uwandani, 2022

Nukuu hii ni ishara ya raha ya uradidi wa vitabu vya fasihi katika shule za sekondari nchini Tanzania. Hii ni kwa sababu uradidi huo umefanya mambo kuwa mepesi kuanzia ufundishaji, ujifunzaji na hatimaye kutoa matokeo mazuri kwa wanafunzi katika mtihani wa taifa. Kwa mfano, katika Jedwali Na. 4 ufaulu wa kidato cha nne umeonekana kuongezeka kila mwaka kutoka asilimia 91 mwaka 2019 hadi asilimia 95 mwaka 2021. Kwa upande wa kidato cha sita, kwa miaka minne mtawalia (2019-2022) ufaulu umebaki kuwa asilimia 100. Hivyo, ili kupata uhalisia wa matokeo hayo ni wakati mwafaka sasa kutekeleza mabadiliko ya vitabu vya fasihi katika ngazi hizo.

### 5.2 Karaha ya Uradidi wa Vitabu

Mbali na raha zilizobainishwa, utafiti huu umebaini kuwa uradidi wa vitabu vya fasihi nchini Tanzania una karaha. Karaha hizo ni pamoja na wanafunzi kukariri kikasuku, kutokomea kwa tabia ya usomaji wa vitabu, kutotoa ushindani kwa waandishi, kuwanyima haki waandishi, kuua vipaji vya waandishi chipukizi, kutokwenda na wakati na kuidumaza fasihi. Karaha hizo zimewasilishwa na zinachambuliwa kwa mujibu wa mwongozo wa Nadharia ya Uhalisia kupitia dhima ya nadharia hiyo kama ifuatavyo:

#### 5.2.1 Wanafunzi Kukariri Kikasuku

Somo la fasihi linapaswa limwandae mwanafunzi kuelewa utamaduni wake na tamaduni nyingine, kuibua kipawa cha uandishi wa kubuni, kuimarisha udadisi wa kusaili mambo yanayomzunguka, na kuikomaza lugha ya mwanafunzi. Hayo yote yanaweza yasipatikane ikiwa kutakuwa na uradidi wa vitabu vya fasihi. Hii ni kwa sababu wanafunzi wamekuwa wakikariri kikasuku tahakiki na mapitio ya vitabu teule vinavyodumu zaidi ya muongo mmoja. Hili lilithibitishwa na mmoja wa watoataarifa anayesema:

> Sisi wanafunzi huwa hatusomi vitabu kwa sababu tahakiki zimejaa tele madukani. Kama huna pesa unaweza kutumia tahakiki za watangulizi wako shuleni kwani wakiondoka wanatuachia. Hata walimu nao wanatumia tahakiki hizo, sijui kama wanasoma vitabu nao
> **Chanzo:** Data za Uwandani, 2019.

Hayo ni maelezo yaliyotolewa na mtoataarifa. Mwanafunzi mwenyewe anakiri kwamba huwa hawasomi vitabu kwa kuwa tahakiki zimejaa madukani. Hii ni kama Waswahili wasemavyo: ‘maziwa unapata, ya nini kufuga ng’ombe?’ Ikumbukwe kuwa mafunzo yalipaswa kuzingatia uhusika wa wanafunzi kuhusu mustakabali, masilahi na shughuli zao; nini wanataka kufanya baada ya kujifunza. Kujifunza fasihi hakupaswi kutazamwa kama somo la shule la kufaulu mtihani tu. Ujifunzaji huo pia unapaswa kutazamwa kama kujifunza somo kuhusu maisha baada ya shule. Hayo yote yangewezekana ikiwa mikakati imara itawekwa na kufuatiliwa ipasavyo. Mikakati hiyo ni pamoja na kupiga marufuku tahakiki za wachuuzi wengine wa lugha ya Kiswahili, ambao wanadhamiria kujaza mifuko yao senti bila ya kujali mustakabali wa wahitimu.

#### 5.2.2 Kuitokomeza Tabia ya Usomaji wa Vitabu

Katika nchi ya Tanzania tabia ya usomaji wa vitabu imekuwa chini tangu zama. Kutokana na hilo, Madumulla (2009:19) aliuliza swali: “Tufanye nini ili kuharakisha ujenzi wa jadi ya usomaji?” Katika kulijibu swali hilo, Madumulla (*keshatajwa*) alipendekeza mambo mbalimbali, miongoni mwayo lilikuwa:

> Kushinikiza serikali iimarishe tasnia ya vitabu kwa kuenzi na kusaidia uandishi, uchapishaji, uchapaji, na usomaji, kwani kwa jinsi hiyo njia ya kuelekea kwenye jadi ya usomaji itakuwa inaimarishwa (uk. 19).

Maelezo hayo ya Madumulla yametoa dira ya namna ya kuimarisha tabia ya usomaji wa vitabu kwa ngazi ya kitaifa. Hata hivyo, kinachotokea shuleni ni kuwa wanafunzi na mwalimu wao hupitia tahakiki za watu wengine pasi kusoma vitabu, wakati mwalimu anapaswa kuhakikisha kwamba wanafunzi wamesoma kwanza vitabu teule kabla ya uchambuzi wa vitabu hivyo darasani. Mwalimu anaweza kuthibitisha usomaji wa wanafunzi kwa kuwaagiza kutoa muhtasari kabla ya uhakiki lakini hili litawezekana vipi wakati kuna tahakiki na mapitio ya vitabu hivyo teule kwa zaidi ya muongo mmoja hivi sasa? Wanafunzi, moja kwa moja, wanaishia kusoma tahakiki na mapitio hayo. Hii ni kwa kuwa, katika hali ya kawaida, hakuna mtu anayetaka usumbufu wa kusoma kitabu ukurasa mmojammoja hadi mwisho wakati ufupisho na uchambuzi wake umejaa tele madukani.

### 5.2.3 Kutotoa Ushindani kwa Waandishi

Ushindani hukaribisha ufanisi katika ubora na usasa. Kila mwandishi hujipambanua dhidi ya washindani wake. Hili halina budi kufanywa hata katika uteuzi wa vitabu vya fasihi katika shule za sekondari nchini. Uradidi wa vitabu hautoi fursa hiyo kwani waandishi ambao vitabu vyao vimeshateuliwa katika mtaala huwa hawana wahaka wala wasiwasi wa kutolewa katika nafasi hiyo. Vitaendelea kubaki tu, aliyemo yumo na asiyekuwamo hana nafasi ya kuwamo. Hili limethibitishwa na mmoja wa watoataarifa wetu ambaye anasema:

> Kwa hakika wanadumaza ushindani wa uandishi hapa kwetu Tanzania. Hii ni kwa sababu aliyemo yumo na asiyekuwemo haoni ufalme wa milele. Kwa maana waliotutangulia katika uandishi wanabaki wao kwa wao, bali hata baadhi yao hawamo katika mtaala wa taifa.
> **Chanzo:** Data za Uwandani, 2019.

Hoja anayoisimamia hapa ni kuwa kuruhusu soko huria ndiyo chachu ya mafanikio ya shughuli yoyote ile. Hivyo, ubadilishaji wa vitabu teule mara kwa mara, ungeweza kukuza ushindani na kuimarisha uandishi kwani kila mwandishi angejibidiisha kutunga kazi bora. Hata Nadharia ya Uhalisia inaitaka kazi ya fasihi iangalie changamoto na kuchunguza chanzo chake kwa minajili ya kutafutia suluhisho. Hivyo, suluhisho la changamoto ya ukosefu wa ushindani kwa waandishi ni kuruhusu mabadiliko ya vitabu teule mara kwa mara.

### 5.2.4 Kuwanyima Haki Waandishi

Mwandishi ana wajibu wa kuiandikia jamii yake kutokana na mazuri au mabaya yanayoikabili jamii hiyo. Wakati mwingine hata kuitabiria chungu na/au tamu zinazotarajiwa kujiri baina yake. Suala hilo hurejeshwa nyuma kwa kumkatisha

tamaa mwandishi kwa kutomuunga mkono kwa njia moja au nyingine. Mtoataarifa anasema:

> Unajua kuna wakati unakuwa na hamu ya kuandika lakini hamu hiyo hukatishwa na vidudu watu, yaani watu wasiojali haki za wengine. Ndiyo haki kwani kila mwandishi ana wajibu wa kuandika na yeye ana haki ya kupewa nafasi katika jamii yake kupitia kwa wenye mamlaka, katika mitaala kwa muktadha huu.
> **Chanzo:** Data za Uwandani, 2019.

Hii ni wazi kuwa uradidi wa vitabu teule vya fasihi vya shule za sekondari kwa zaidi ya muongo mmoja huleta machungu na kuwanyima haki waandishi wengine, wenye ghera na shauku ya kuandika kwa ubunifu mkubwa pia. Inawezekanaje kwa muda wa miaka zaidi ya kumi kitabu hichohicho kinajirejea pasi na kutokeza mpinzani wake? Hii ndio maana ya 'kunyimwa haki ya vitabu vyao kusomwa na wanafunzi' kama mmoja wa waandishi aliye nje ya orodha ya vitabu teule, alivyoiita. Hivyo, suala hili halina budi kutafutiwa ufumbuzi kwa mustakabali mwema wa waandishi, wanafunzi na fasihi kwa ujumla.

### 5.2.5 Kuua Vipaji vya Waandishi Chipukizi

Bila ya shaka sanaa haituami, kila siku inasonga mbele na kupata wafuasi hasa kwa wanagenzi, wenye damu changa inayochemka. Ifahamike kuwa uanagenzi wao usichukuliwe kama turufu ya kuwaviza au kuwatweza. Hii ni kwa sababu hata mwandishi nguli, Shaaban Robert, naye alianza kama mwanafunzi hatimaye akawa nguli, na leo hii anaitwa baba wa fasihi ya Kiswahili. Mtoataarifa mmoja alisema:

> Hata mbuyu ulianza kama mchicha. Ingawa si wanafunzi wote katika fasihi wanaotambaa; wako wanaoanza kwa kuruka kama walivyo nguli wakongwe. Kwani hakuna miongoni mwa hao nguli wakongwe waliotoa kazi ya kwanza tu wakang'aa na kujulikana kwa kazi hiyohiyo?
> **Chanzo:** Data za Uwandani, 2019.

Maelezo anayoyatoa mtoataarifa huyu yana ukweli kwani, mathalani, Haji Gora kupitia diwani ya *Kimbunga* na Abdulatif Abdallah kupitia diwani ya *Sauti ya Dhiki*, wamepata umaarufu kwa kazi zao za kwanza katika uandishi. Basi, kwa nini kwa hawa waandishi chipukizi wa leo isiwezekane? Ni wazi kuwa kutowapa nafasi ya kusomwa kazi zao kupitia orodha ya vitabu teule ni kuvifunika au kuviua kabisa vipaji vyao. Hivi sasa kuna mashindano mbalimbali ya uandishi wa vitabu vya kifasihi. Kupitia mashindano hayo waandishi chipukizi wameonekana kuchanua kiubunifu. Hivyo, nao wanapaswa wapewe nafasi ya kusomwa kimtaala ili wapate ari na mori wa kuendeleza gurudumu la utunzi wa kazi za fasihi.

### 5.2.6 Kutokwenda na Wakati na Kuidumaza Fasihi

Kazi za fasihi lazima ziende na wakati ili ziendane na mabadiliko yanayojitokeza katika jamii na kuweza kujivumbua kifani na kimaudhui. Kwenda na wakati hakutamnyima nafasi msanii kwa kuachwa nyuma katika ushindani wa kibiashara katika soko huria kwa kuwa kunatoa fursa kwa msanii kujua njia mpya za uzalishaji. Atabaini na kuzitumia njia ambazo zitamvusha yeye na kazi zake dhidi ya uchakavu wa kazi ya kifasihi mbele ya macho ya hadhira. Suala hili lilimsukuma mtoataarifa hata akaeleza akaeleza:

> Baadhi ya vitabu vimepitwa na wakati sipendi kuvitaja kwa majina. Lakini muda wa miaka kumi ni mingi sana kwa mtaala wa fasihi kubaki na vitabu hivyohivyo, kwa sababu hata tawala za kisiasa zinakuwa zimebadilika. Hivyo, mambo ya kiuchumi, kijamii hata kitaaluma yanaweza kuwa yamebadilika. Basi angalau kuwe na mabadiliko ya miaka miwili mitatu.
> **Chanzo:** Data za Uwandani, 2019.

Anachokieleza hapo ni kuwa kwa kuwa jamii inakabiliwa na mabadiliko ya nyanja zote za maisha kutokana na mabadiliko ya wakati, utawala, sera na mitazamo, mitaala nayo haina budi kubadilishwa ili kuendana na mabadiliko hayo. La si hivyo, mitaala hiyo itajikuta inajikongoja wakati jamii imeitangulia kwa kitambo. Kwa mintarafu hiyo, ili kuepukana na kupitwa na wakati huko anakokueleza mtoataarifa huyo, mitaala haina budi kujiepusha na uradidi wa vitabu teule vya fasihi kwa shule za sekondari kwa muda mrefu. Hatimaye, anapendekeza kwamba vitabu hivyo visichukue muda mrefu sana kubadilishwa kama ilivyo hivi vya sasa.

## 6.0 Hitimisho

Ni wazi kuwa raha na karaha ya uradidi wa vitabu teule vya fasihi kwa shule za sekondari nchini Tanzania kupitia makala haya ni kama zinalingana. Tofauti ni ndogo. Matokeo yameonesha kuwapo kwa raha tano na karaha sita za uradidi wa vitabu hivyo. Hivyo, wenye mamlaka na wadau wa fasihi ya Kiswahili waangalie namna ya kufanya mabadiliko au mpishano wa uteuzi wa vitabu vya fasihi katika shule za sekondari nchini Tanzania kwa minajili ya mustakabali mwema wa wahitimu, walimu, waandishi wa vitabu vya fasihi na fasihi yenyewe kwa ujumla. Hii ni kwa sababu baadhi ya waandishi ambao vitabu vyao havimo katika mtaala wa elimu huenda wakakata tamaa, wanafunzi nao wanaweza kuishia kusoma tahakiki tu na walimu kukosa ari ya kujisasisha kivitabu.

Hapa ifahamike kuwa mchakato wa uteuzi wa vitabu teule usifanywe kiholela ili vilivyopo vipate kubadilishwa, bali, upembuzi wa kina unapaswa kufanyika ili kuvigundua vyenye sifa kulingana na matakwa ya mtaala, wakati, rika la wanafunzi pamoja na ubunifu wa kifasihi. Aidha, waandishi, wachapishaji na wachapaji nao hawana budi kuzingatia maadili ya taaluma zao pamoja na kanuni za nchi, ili kuzalisha vitabu vyenye ubora vinavyoweza kuibua vipaji vya uandishi, kujitambua

na kutatua changamoto zinazoisibu jamii ya leo. Haya yakifanyiwa kazi, wadau wote wa elimu na fasihi ya Kiswahili wataridhika na mustakabali wa wahitimu utakuwa mwema.

## Marejeleo

Baraza la Mitihani la Tanzania (2019) *Taarifa ya Uchambuzi wa Majibu ya Watahiniwa katika Mtihani wa Kidato cha Sita (ACSEE) 2019, 121 Kiswahili*. NECTA: Dar es Salaam.

Baraza la Mitihani la Tanzania (2020) *Taarifa ya Uchambuzi wa Majibu ya Watahiniwa katika Mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE) 2019, 021 Kiswahili*. NECTA: Dar es Salaam.

Baraza la Mitihani la Tanzania (2020) *Taarifa ya Uchambuzi wa Majibu ya Watahiniwa katika Mtihani wa Kidato cha Sita (ACSEE) 2020, 121 Kiswahili*. NECTA: Dar es Salaam.

Baraza la Mitihani la Tanzania (2021) *Taarifa ya Uchambuzi wa Majibu ya Watahiniwa katika Mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE) 2020, 021 Kiswahili*. NECTA: Dar es Salaam.

Baraza la Mitihani la Tanzania (2021) *Taarifa ya Uchambuzi wa Majibu ya Watahiniwa katika Mtihani wa Kidato cha Nne (ACSEE) 2021, 121 Kiswahili*. NECTA: Dar es Salaam.

Baraza la Mitihani la Tanzania (2022) *Taarifa ya Uchambuzi wa Majibu ya Watahiniwa katika Mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE) 2021, 021 Kiswahili*. NECTA: Dar es Salaam.

Baraza la Mitihani la Tanzania (2022) *Taarifa ya Uchambuzi wa Majibu ya Watahiniwa katika Mtihani wa Kidato Cha Sita (ACSEE) 2022, 121 Kiswahili*. NECTA: Dar es Salaam.

Karelis, C. (1979) *Hegel's Introduction to Aesthetics.* London: Clarendon Press.

Madumulla, J.S. (2009) *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Dar es Salaam: Mture Educational Publishers.

Mulokozi, M.M. (2019) "Pambazuko la Taaluma ya Fasihi ya Kiswahili Afrika Mashariki: 1968-1980". Katika F. Aiello na R. Gaudioso (Wah.) *Lugha na Fasihi*. Napoli: Unior Press. kur. 19-30.

Ntarangwi, M. (2004) *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Augustana College: Rock Island.

Wafula, R.M. (2007) *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi, Sai Industries Limited.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (2010) *Muhtasari wa Kiswahili, Kidato cha I-IV*. Dar es Salaam: Taasisi ya Elimu Tanzania.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (2010) *Muhtasari wa Kiswahili, Kidato cha V-VI*. Dar es Salaam: Taasisi ya Elimu Tanzania.

Zombwe M.G. (2011) *Nani Huamua Watoto wetu Wajifunze Nini? Ripoti ya Utafiti kuhusu Uhusiano wa Ubora wa Mitaala na Utoaji Elimu Bora*. Dar es Salaam: Haki Elimu.